



SHERIA YAMAKISIO NA MATUMIZI YA MWAKA 2016
MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU MAELEZO

1. Jina fupi.
2. Tafsiri.
3. Utoaji wa Shilingi 841,477,500,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.
4. Makisio ya fedha zilizokubalika.
5. Uwezo wa Waziri kukopa.
6. Uwezo wa Waziri wa maombi ya ziada.
7. Marejesho ya mkopo na riba.
8. Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo.
9. Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendelezo.

JADWELI



**SHERIA NAMBA 2 YA 2016
NIMESAINI**

Alhaji

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI**

5 Julai, 2016

**SHERIA YA KUIDHINISHA MAKISIO NA MATUMIZI YA SHILINGI
BILLIONI MIA NANE NA AROBAINI NA MOJA, MIA NNE NA SABINI
NA SABA MILLIONI NA LAKI TANO KUTOKA MFUKO MKUU WA
HAZINA YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA SIKU YA
TAREHE THELATHINI JUNI, MWAKA WA ELFU MBILI NA KUMI NA
SABA NA KURUHUSU UTOAJI NA UHAULISHAJI WA FEDHA HIZO
PAMOJA NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO**

UMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

- Jina fupi. 1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Makisio na Matumizi ya mwaka 2016.
- Tafsiri. 2. Tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria hii yatakuwa na maana iliyoelezwa katika Sheria ya Fedha za Umma.
- Utoaji wa Shilingi 841,477,500,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. 3. Idara ya Hazina, Wizara ya Fedha inaweza kutoa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kiasi cha Shilingi Billioni Mia Nane Na Arobaini Na Moja, Mia Nne Na Sabini Na Saba Millioni Na Laki Tano kwa matumizi ya huduma kumalizikia mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2017.



Makisio
ya fedha
zilizokubalika.

4. Kiasi cha fedha kilichotolewa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii kitatumika kwa matumizi yale tu na kima tu kilichoelekezwa katika Jadwali za Sheria hii.

Uwezo wa
Waziri
kukopa.

5.(1) Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Fedha anaweza kukopa wakati wowote ule lakini sio zaidi ya tarehe 30 Juni, 2017 ikiwa ndani au nje ya Zanzibar kiasi chochote cha fedha ambacho hakitozidi kiasi kilichokubalika au kusemekana kukubalika kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii kwa njia ya mikopo kwa taratibu za Benki au taratibu nyengine, kwa mpango ule atakaona unafaa na atalipa fedha hizo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

(2) Fedha zozote zilizokopwa chini ya kijifungu (1) cha kifungu hiki zitawekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na zitakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na zitapatikana na kutumika kwa mujibu wa hali ya fedha inavyoruhusu.

(3) Fedha zozote zilizokopwa chini ya kijifungu (1) cha kifungu hiki zitapaswa kulipwa si zaidi ya tarehe 30 Juni, 2017, na fedha zitakazohitajika kwa malipo ya faida (riba) ya mkopo zitatolewa na kulipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

(4) Uwezo aliopewa Waziri mwenye dhamana na mambo ya Fedha wa Zanzibar chini kijifungu cha (1) cha kifungu hiki itakuwa ni nyongeza ya uwezo wake chini ya Sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Ruzuku Nam. 5 of 1978.

Uwezo wa
Waziri wa
maombi ya
ziada.

6.(1) Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Fedha ikiwa ataona ni manufaa kwa Taifa kutoa matumizi ya ziada kwa Wizara au Idara yoyote ya Serikali ikiwa ni zaidi ya fedha zilizokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa au kwa madhumuni ya huduma nyengine yoyote na itakuwa ni hasara kwa Taifa kusubiri mpaka pale zitakapotolewa tena na Baraza la Wawakilishi, bila ya kujali masharti ya Sheria hii au Sheria nyengine yoyote anaweza kuidhinisha matumizi ya ziada ambayo yatatumika kwa mujibu wa kasma inayohitajika.



(2) Waziri mwenye dhamana na mambo ya Fedha atakapoidhinisha maombi ya kiasi chochote cha fedha chini ya kifungu hiki mara tu baada ya kuruhusu maombi hayo ya ziada atawasilisha nyongeza ya makisio hayo mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa maelezo ya nyongeza hiyo kama hali itakavyokuwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu 106 (2) cha Katiba ya Zanzibar, 1984 ikiwa ni nyongeza ya matumizi ya ziada.

(3) Waziri mwenye dhamana na mambo ya Fedha anaweza kukasimu uwezo wake alionao chini ya kifungu hiki kwa Afisa yeyote kwa mujibu wa masharti atakayoona yanafaa.

Marejesho
ya mkopo
na riba.

7. Kiasi cha fedha kitakachohitajika wakati wowote kama malipo ya mkopo na riba kuhusiana na fedha za mwaka 2016/2017 (Shiligi 27,979,299,600/=) zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Kukubaliwa
kwa
Mipango
ya
Maendeleo.

8. Mipango ya maaendeleo iliyoainishwa kwenye Jadweli inakubaliwa kwa mwaka 2016/2017.

Kukubaliwa
kwa
Fedha
zilizopitishwa
kwa
matumizi
ya
maendeleo.

9. Fedha zilizokubaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria hii zinaidhinishwa kwa matumizi ya maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye Jadweli ya Sheria hii na yatatumika kwa kiasi cha matumizi yale tu yalioainishwa kwenye Jadweli ya Sheria hii.

JADWELI

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO 2016/2017

Tshs, '000'



Fungu/ Kitungu	Wizara/Programu	MATUMIZI KAWAIDA			MATUMIZI YA MAENDELEO		JUMLA
		Mshahara	Uendeshaji wa Ofisi	Ruzuku	SMZ	WAHISANI	
A01	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	3,080,300	1,917,900		500,000		5,498,200
PA0101	Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na Kutaratisha Mawasiliano Kuu	1,739,454	627,900		500,000		2,867,354
PA0102	Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Uratibu wa Zanzibar Vanaosishi Nchi za Nje	104,521	399,999				504,520
PA0103	Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu	1,236,325	890,001				2,126,326
A02	Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi	789,900	702,100				1,492,000
PA0201	Usimamizi wa Majukumu ya Kikabla na Kisheru ya BLM na IMTC		176,490				176,490
PA0202	Utumishi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	789,900	525,610				1,315,510
C01	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais	3,271,900	3,245,000		1,210,000	8,120,400	15,847,300
PC0101	Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	506,106	250,360				756,466
PC0102	Uratibu wa shughuli za Serikali	1,169,803	1,859,223		210,000	8,120,400	11,359,426
PC0103	Usimamizi wa shughuli za Ujigaji Chapa	480,580	393,360				873,940
PC0104	Uongozi na Utawala	1,115,411	742,057		1,000,000		2,857,468
C02	Baraza la Wawakilishi	8,373,800	8,764,700				17,138,500
PC0201	Kutunga sheria, kupitisha Bajeti na Kusimamia taasisi za Serikali		6,542,950				6,542,950
PC0202	Uongozi na utawala wa Baraza la Wawakilishi	8,373,800	2,221,750				10,595,550
C03	Tume ya Uchaguzi	1,065,400	294,800				1,360,200
PC0302	Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi	1,065,400	294,800				1,360,200
C04	Tume ya Kitafu ya Kuratibu na Udhhibiti wa Dawa za Kulevya	205,800	234,100				439,900
PC0401	Udhhibiti wa Dawa za Kulevya		88,813				88,813
PC0402	Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya	205,800	145,287				351,087
C05	Tume ya Ukimwi	270,700	416,100		20,000	499,376	1,206,176
PC0501	Kuratibu Mutiko wa taifa wa UKIMWI		222,289		20,000	499,376	741,665
PC0502	Utawala na Uendeshaji	270,700	193,811				464,511
D01	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	1,807,800	1,153,500	1,500,000	18,000,000		22,461,300
PD0101	Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	610,378	281,262	1,500,000			2,391,640
PD0102	Uratibu wa Idara Maalum za SMZ		44,993				44,993
PD0103	Usimamizi wa Utumishi wa Idara Maalum		115,232				115,232
PD0104	Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ	1,197,422	712,013		18,000,000		19,909,435
D02	Jeshi la Kujenga Uchumi	10,616,500	839,900				11,456,400
PD0201	Uzalendo, Uzalishaji, Kazi za amali na Michezo		49,000				49,000



Fungu/ Kifungu	Wizara/Programu	MATUMIZI KAWAIDA			MATUMIZI YA MAENDELEO		JUMLA
		Mshahara	Uendeshaji wa Daga	Ruzuku	SMZ	WAHISANI	
PD0202	Ulinzi, Mipango na Uendeshaji wa JKU	10 616,500	790,900				11,407,400
D03	Chuo cha Mafunzo	7,586,600	1,383,400		250,000		9,220,000
PD0301	Huduma za Urekebishaji Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo		968,895		250,000		1,218,895
PD0302	Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo	7,586,600	414,505				8,001,105
D04	Kikosi Maalum cha Kuruzia Magendo	12,686,100	2,448,400		1,242,000		16,376,500
PD0401	Ulinzi na Uzulaji wa Magendo		964,700				964,700
PD0402	Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM	12,686,100	1,483,700		1,242,000		15,411,800
D05	Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	4,423,700	487,400				4,911,100
PD0501	Uoaji wa huduma za Zimamoto na Uokozi		268,404				268,404
PD0502	Kukuza huduma za kiutawala, mafunzo kutendaji, mipango na Uongozi	4,423,700	218,996				4,642,696
D06	Kikosi cha Valantia	6,214,300	425,600		827,200		7,527,100
PD0601	Amani na Uthivu kwa Taifa, Rala na Mali zao		358,000				358,000
PD0602	Usimamizi na utawala wa Kikosi cha Valantia	6,214,300	67,600		827,200		7,169,100
D07	Mkoa wa Mjini Magharibi	915,100	722,100				1,637,200
PD0701	Urathibu wa shughuli za maendeleo		240,388				240,388
PD0702	Usimamizi na Utawala wa Mkoa	915,100	481,712				1,396,812
D08	Mkoa wa Kusini Unguja	864,700	398,900				1,263,600
PD0801	Urathibu wa shughuli za maendeleo ya Mkoa wa Kusini Unguja		193,727				193,727
PD0802	Uendeshaji na utawala Mkoa wa Kusini Unguja	864,700	205,173				1,069,873
D09	Mkoa wa Kaskazini Unguja	872,400	401,000				1,273,400
PD0901	Urathibu wa shughuli za maendeleo ndani ya Mkoa		213,952				213,952
PD0902	Utawala na uendeshaji	872,400	187,048				1,059,448
D10	Mkoa wa Kusini Pemba	723,000	413,400		782,026		1,918,426
PD1001	Kurathibu shughuli za maendeleo katika Mkoa		50,938				50,938
PD1003	Mipango na utawala katika Mkoa	723,000	362,462		782,026		1,867,488
D11	Mkoa wa Kaskazini Pemba	798,000	445,800		330,500		1,574,300
PD1101	Kurathibu shughuli za maendeleo katika Mkoa		86,792				86,792
PD1103	Mipango na utawala katika mkoa	798,000	359,008		330,500		1,487,508
D12	Ofisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho	812,400	1,277,500				2,089,900
PD1201	Kusajili na kutoa vitambulisho kisheria		75,000				75,000
PD1202	Utumishi na uendeshaji Afisi ya usajili na kadi za utambulisho	546,300	939,800				1,486,100
PD1203	Kusajili matukio ya kijamii	266,100	262,700				528,800
F01	Wizara ya Fedha na Mipango	27,745,900	4,271,100	25,721,000	6,630,000	3,881,529	68,249,529



Fungu/Kitungu	Wizara/Programu	MATUMIZI KAWAIDA				MATUMIZI YA MAENDELEO		JUMLA
		Mshahara	Uendeshaji wa Ofisi	Ruzuku	SMZ	WAHISANI		
PF0101	Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma	25,705,925	1,403,492	23,087,000	1,030,000	2,970,630	54,197,047	
PF0102	Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma	348,776	114,806	734,000	5,570,000		6,767,582	
PF0104	Mipango na uendeshaji sekta ya Fedha	1,691,198	2,752,802	1,900,000	30,000	910,899	7,284,899	
F02	Mfuko Mkuu wa Serikali	1,229,300	82,300,600				83,529,900	
PF0201	Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali	1,229,300	82,300,600				83,529,900	
F03	Tume ya Mipango	993,000	1,105,100	1,312,200	870,000	1,631,678	5,911,978	
PF0301	Kuratibu Mipango ya Kiajira na Maendeleo ya Watenda kazi	358,175	400,000		370,000	1,631,678	2,759,853	
PF0302	Usimamizi wa Uchumi Mkuu	312,100	250,000	1,312,200	500,000		2,374,300	
PF0303	Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango	322,725	455,100				777,825	
G01	Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	3,058,000	1,824,300	1,268,900	900,000	840,195	7,891,395	
PG0103	Utawala Bora, Haki za Binaadamu na Usalama wa Watumishi wa Umma	145,645	202,975				348,620	
PG0104	Usimamizi wa Masuala ya Dini	210,482	123,225				333,707	
PG0105	Mipango na Utawala	1,919,165	860,196	1,268,900	900,000	840,195	5,768,456	
PG0106	Usimamizi wa Rasimwali Watu, Mfumo na mjiundo ya Taasisi	339,721	167,604				507,325	
PG0107	Uimarishaji wa kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali	442,987	470,300				913,287	
G02	Mahkama Kuu	4,097,700	1,134,700				5,232,400	
PG0201	Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki	2,237,845	595,078				2,832,923	
PG0202	Usimamizi wa Shughuli za Uendeshaji na Utawala	1,859,855	539,622				2,399,477	
G03	Mwanasheria Mkuu Zanzibar	517,900	550,700				1,068,600	
PG0301	Maguuzi ya utokaji wa huduma za Sheria	384,874	225,912				610,786	
PG0302	Utawala na Usimamizi wa Ofisi ya Mwanasheria	133,026	324,788				457,814	
G04	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka	1,180,400	469,200	54,800			1,704,400	
PG0401	Uendeshaji na usimamizi wa kesi za jinai	984,837	178,732				1,163,569	
PG0402	Mipango na uendeshaji katika afisi ya mkurugenzi mashitaka	195,563	290,468	54,800			540,831	
G05	Tume ya Kurekebisha Sheria	192,500	316,000				508,500	
PG0501	Kuzifanya mapito ya shera	192,500	190,000				382,500	
PG0502	Utawala na Uendeshaji		126,000				126,000	
G06	Ofisi ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1,158,200	1,086,600				2,244,800	
PG0601	Udhidhi wa Fedha na Rasimwali za Umma	626,801	479,964				1,106,765	
PG0602	Utawala na Uendeshaji wa Udhidhi na Ukaguzi	531,399	606,636				1,138,035	
G07	Mamlaka ya Kuzuya Rushwa na Uhujiu wa Uchumi	456,300	480,000				936,300	
PG0701	Kupunguza Vilendo vya Rushwa na Uhujiu wa Uchumi		117,523				117,523	



Fungu/ Kifungu	Wizara/Programu	MATUMIZI KAWAIDA			MATUMIZI YA MAENDELEO			JUMLA
		Mshahara	Uendeshaji wa Ombi	Ruzuku	SMZ	WAHISANI		
PG0702	Utawala na Uendeshaji katika Mapambano ya Rushwa na Uhujiumu wa Lebuni	456,300	362,477				818,777	
G08	Kamisheni ya Utumishi wa Umma	349,100	460,100				809,200	
PG0801	Usimamizi wa Mifumo ya Rasilmali watu katika Utumishi wa Umma	198,900	170,281				369,181	
PG0802	Utawala na Uendeshaji Kamisheni ya Utumishi	150,200	289,819				440,019	
G09	Tume ya Utumishi Serikalini	145,200	272,700				417,900	
PG0901	Usimamizi Wa Watumishi Serikalini		181,420				181,420	
PG0902	Utawala na Uendeshaji Wa Tume ya Utumishi Serikalini	145,200	91,280				236,480	
H01	Wizara ya Aya	17,332,400	11,893,300	1,496,600	4,900,000	23,606,255	59,228,555	
PH0101	Huduma za Kinga na Elimu ya Aya	6,065,458	599,931		250,000	20,106,255	27,021,644	
PH0102	Huduma za Tiba	2,051,551	8,736,629		4,150,000	3,500,000	18,438,180	
PH0103	Usimamizi wa Sera za Aya na Utawala	9,215,391	2,556,740	1,496,600	500,000		13,768,731	
H02	Hospitali ya Mhazi Mmoja	7,470,800	1,135,000				8,605,800	
PH0201	Huduma za Uchunguzi na Matibabu		563,685				563,685	
PH0202	Uongozi na Utawala	7,470,800	571,315				8,042,115	
J01	Wizara ya Habari, Utalii, Uamaduni na Michezo	2,724,900	1,888,000	3,958,600	1,000,000	5,597,500	15,169,000	
PJ0101	Maendeleo ya Habari na Utangazaji	208,219	112,170	3,340,406			3,660,795	
PJ0102	Maendeleo ya Uamaduni, Utalii na Michezo	1,037,460	509,483	618,194	400,000	5,597,500	8,162,637	
PJ0103	Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Uamaduni, Utalii na Michezo	1,479,221	1,266,347		600,000		3,345,568	
J02	Kamisheni ya Utalii	576,100	536,800				1,112,900	
PJ0201	Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii		208,505				208,505	
PJ0202	Kuratibu na kusimamia maendeleo ya utalii	576,100	328,295				904,395	
K01	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	66,142,200	11,467,300	15,347,600	1,550,000	45,681,295	140,188,395	
PK0101	Elimu ya Maandalizi na Msingi	25,083,891	4,891,006.0		350,000	5,556,562	35,880,459	
PK0102	Elimu ya Sekondari	18,763,440	1,192,891.0		200,000	27,144,997	47,301,328	
PK0103	Elimu ya juu	980,832	207,900.0	12,351,820			13,540,552	
PK0104	Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali	554,170	209,673.0	1,228,010	1,000,000	12,980,736	15,972,589	
PK0105	Ubora wa Elimu	294,997	386,449.0	1,725,770			2,407,216	
PK0106	Uongozi wa Elimu	20,464,870	4,579,382	42,000			25,086,252	
L01	Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	10,955,400	4,236,400	551,500	1,066,000	32,166,000	48,977,300	
PL0101	Maendeleo ya Kilimo	3,711,412	2,167,832	551,500	185,000		6,515,744	
PL0102	Maendeleo ya Rasilmali za Msttu na Maliasili Zisizorejeshaka	1,421,436	246,000				1,667,436	
PL0103	Maendeleo ya Mifugo	1,320,496	253,500		186,750		1,780,746	
PL0104	Maendeleo ya Uvuvi	611,409	270,000		218,215	18,317,103	19,416,727	



Fungu/Kitungu	Wizara/Programu	MATUMIZI KAWAIDA			MATUMIZI YA MAENDELEO		JUMLA
		Mshahara	Uendeshaji wa Dise	Ruzuku	SMZ	WAHISANI	
PL0105	Mipango na Usimamizi wa Kilimo, Matisasi, Mifugo, na Uvuvi	3,890,647	1,299,068		478,035	13,848,897	19,516,647
N01	Wizara ya Ardhii, Maji, Nishati na Mazingira	3,767,600	1,123,300	4,664,500	3,810,000	44,090,786	57,456,186
PN0101	Mipango na Utawala wa Ardhii, Maji, Nishati na Mazingira	1,882,022	460,424				2,342,446
PN0102	Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhii	1,143,239	381,588		50,000	700,245	2,275,072
PN0105	Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati	283,341	61,988	4,664,500	3,760,000	40,208,366	48,978,195
PN0106	Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi	458,998	219,300			3,182,175	3,860,473
P01	Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	4,265,300	1,055,800	1,003,000	25,080,000	157,150,000	188,554,100
PP0101	Miundombinu na huduma za Usafiri wa Barabara	1,540,897	265,071				1,805,968
PP0102	Uhitadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi	297,765	74,400	360,900			733,065
PP0103	Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)	223,471	112,789				336,260
PP0104	Mipango na Utawala katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	2,203,167	603,540	642,100	25,080,000	157,150,000	185,678,807
Q01	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Wazito	2,241,000	8,097,500		700,000	1,065,960	12,104,460
PQ0101	Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi		127,540		400,000		527,540
PQ0102	Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji		40,090			450,000	490,090
PQ0103	Kuimarisha huduma za Ustawi		4,494,480		300,000	615,960	5,410,440
PQ0104	Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, WWAototo	2,241,000	3,306,189				5,547,189
PQ0105	Kuratibu uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira na Usimamizi wa Utekelezaji wa Shaha		129,201				129,201
R01	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	1,535,700	1,346,500	1,002,200	2,500,000	500,000	6,884,400
PR0101	Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	1,205,217	820,088				2,025,305
PR0102	Maendeleo ya Viwanda na Ujiasimamili	87,684	166,741		100,000		354,425
PR0103	Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara	242,800	359,671	473,199	1,400,000	500,000	2,975,670
PR0104	Viwango na Tathmini ya Uboora			529,000	1,000,000		1,529,000
	Jumla Kubwa	223,573,300	163,022,600	58,993,426	71,057,200	324,830,974	841,477,500

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi, tarehe 26 Juni, 2016.


RAYA ISSA MSELLEM
KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR